MAONI YA MASHIRIKA YASIYO YAKISERIKALI

SHERIA ZA UCHAGUZI NA VYAMA VYA SIASA

JULAI 2023

Baraza la Taifa la NGOs

National Council of NGOs

NaCoNGO

Imefadhiliwa na

FCS FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY

A. UTANGULIZI

Kwa mwaliko wa Msajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Baraza la Taifa ya Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali (NaCONGO) limeratibu wadau na wanachama wake kuandaa mapendekezo ya Sheria Mpya ya Tume ya Uchaguzi, 2023; Marekebisho ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura Namba 278; Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura Namba 258; na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge Madiwani na viongozi wa Serikali za Mitaa, 2023. Mapendekezo haya yamekusanywa kutoka kwa wadau na wanachama wa NaCONGO na baadaye kuandikwa na kujumuishwa na kikundi kazi cha wajumbe wateule wa ngazi ya Taifa ambao walipendekezwa kutokana na utaalam na uzoefu wao katika masuala ya Sheria za Uchaguzi na wakakubali kujitolea kufanya kazi hiyo. Kwa moyo wao, NaCONGO inawashukuru sana wana AZAKI hao.

B. JEDWALI LA MAPENDEKEZO

1. SHERIA MPYA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI YA MWAKA 2023			
Na.	**SUALA AU JAMBO MUHIMU**	**MAONI**	**SABABU**
1.	Jina la Tume ya Uchaguzi.	Jina liwe “ Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi”	Kuleta dhana ya uhuru na mamlaka kwa Tume bila kuingiliwa, kuelekezwa au kuagizwa na mtu, chombo au mamlaka nyingine katika utendaji wa majukumu yake. Uhuru wa Tume uzingatie nyanja za Kimuundo, Kimajukumu na Kibajeti.
2.	Muundo na Uhuru wa Tume	Tunapendekeza Muundo wa Tume uwe katika Sehemu mbili, 1. Usimamizi wa Tume; sehemu hii iundwe na wajumbe tisa (9)	Kutenganisha majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

		pamoja na mwenyekiti wa Tume ambao jukumu kubwa ni kusimamia utendaji wa Tume. 2. Utendaji wa Tume.	
3.	Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.	Tunapendekeza majukumu ya nyongeza kama ifuatavyo: 1. Kuratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Serikali za Mitaa. 2. Kuratibu na kusimamia uchaguzi wa wawakilishi wa Tanzania katika vyombo mbalimbali vya uwakilishi wa kikanda (EALA, SADC & PAP). 3. Kuwa na mamlaka ya kuendesha kura za maoni (referendum) katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 4. Kutoa elimu endelevu ya mpiga kura mara kwa mara angalau mara	Sababu ya mapendekezo ya majukumu ya nyongeza: 1. Shughuli zote za uchaguzi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba hii ziratibiwe na kusimamiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuwa ndiyo chombo pekee chenye utaalamu na uzoefu wa mambo ya uchaguzi. 2. Kuimarisha demokrasia ya uwakilishi wa moja kwa moja kikanda (EALA, SADC & PAP). 3. Kuziba ombwe la uratibu wa kura za maoni/maamuzi (referendum) za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Kujifunza kutoka Zanzibar) 4. Kukuza uelewa wa wananchi kuhusu uchaguzi na haki ya kupiga kura ili kuongeza mwitikio na ushiriki. 5. (a) Tume ya Uchaguzi ndio mamlaka ya kuratibu wadau wa uchaguzi ; (b) Kuimarisha ushiriki wa wadau wa uchaguzi i.e NGOs.

		tatu kwa mwaka kwa makundi yote. 5. Kuratibu wadau wa uchaguzi katika kutoa elimu ya mpiga kura katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 6. Kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura wa uchaguzi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 7. Kuhakiki na kuboresha daftari la kudumu la mpiga kura mara tatu ndani ya miaka mitano.	6. Kusiwepo na chombo chochote chenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi wa JMT kama vile inavyofanya TAMISEMI katika uchaguzi wa serikali za mtaa. 7. Kumuwezesha kila Mtanzania mwenye sifa ya kupiga kura kutimiza haki yake kikatiba.
3.	Utaratibu wa Uteuzi na Utenguzi wa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi	Tunapendekeza kuwe na Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe na Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa. Kamati hii itakuwa na majukumu makubwa mawili (2); Kusajili (recruit) wajumbe wa Tume; Kupendekeza majina kwa Rais ambapo wataapa mbele ya Rais ndani ya siku 30. ya Uchaguzi itakayoundwa na wajumbe wafuatao;	Lengo ni kuweka mchakato wa wazi na wa ushindani utakaopelekea upatikanaji ya wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

		1. Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa Mwenyekiti. 2. Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti. Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu au Jaji wa Mahakama Kuu atakayeteuliwa na Jaji Kiongozi ambaye atakuwa Katibu. Naibu Mwanasheria Mkuu. Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika. Rais wa Chama cha Majaji Wanawake wa Tanzania. Rais wa Chama cha Mawakili Zanzibar. Wawakilishi wawili kutoka kundi la Asasi za Kiraia waliyofanya kazi katika eneo la utawala bora kwa zaidi ya miaka 10 mmoja lazima awe mwanamke. Mwakilishi kutoka Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu, uwakilishi huo uzingatie jinsia. Nafasi ya Wajumbe pamoja na Mkurugenzi wa Tume watatakiwa	

		kufanya maombi ya nafasi hizo kupitia Katibu wa Kamati ya Uteuzi.	
4.	Sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi	1. Awe ni mwanasheria mbobevu aliyefanya kazi kwa muda usiyopungua miaka 15 mfululizo katika nafasi ya Ujaji, Mwanasheria Mwandamizi au Wakili Mkongwe au mwenye sifa zifanazofana na hizo. 2. Asiwe mtu aliyewahi kujihusisha na siasa za vyama kwa muda wa miaka mitano kabla ya kuomba nafasi hiyo.	Kuhakikisha Mkurugenzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ni mtu mbobevu asiyefungamana na chama cha siasa.

5.	Utaratibu wa Vikao vya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.	Tunapendekeza vikao vya wajumbe wa Tume vifanyike mara nne (4) kwa mwaka kwa ajili ya kufanya usimamizi wa kazi za kitendaji za Tume.	Lengo ni kuwa na vikao vya kiutawala kila baada ya miezi mitatu mara nne kwa mwaka.
6.	Chanzo cha fedha za uendeshaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na shughuli za uchaguzi.	Tunapendekeza chanzo cha fedha za uendeshaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi; 1. Itokane na fungu maalamu litakalowekwa na Bunge ambalo si chini ya asilimia 3% ya Bajeti ya Serikali. 2. Misaada kutoka katika vyanzo halali. Fedha hizo zitumike kwa ajili ya mishahara, posho na pensheni pamoja na matumizi ya Tume kwa ajili ya kazi za kitendaji na usimamizi.	Kuweka chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya Tume.
7.	Muundo wa Utumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.	Kuweka muundo uliyowazi unaotenganisha sehemu ya Tume ya Utendaji yaani wafanyakazi wa	Kuimarisha utendaji wa Tume kwa kutenganisha majukumu ya Tume ya Kiutendaji na majukumu ya kiusimamizi.

		Tume na sehemu ya Tume ya Usimamizi yaani Kamisheni ya Tume.	
8.	Kuipa Tume mamlaka ya kutunga kanuni, kuandaa miongozo na kutoa maelekezo.	Tunapendekeza Tume itekeleze mamlaka ya kutunga kanuni kwa ajili ya kutekeleza mambo yafuatayo; 1. Mambo ya kinidhamu ya wafanyakazi wa Tume au wanaofanya kazi kwa niaba ya Tume. 2. Jinsi ya utendaji kazi wa Tume. 3. Namna ya ugatuzi wa madaraka ya Tume.	Kuweka mipaka ya maeneo au mambo ambayo Tume inaweza kutunga kanuni, kuandaa miongozo na kutoa maelekezo.

3. SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI, SURA NAMBA 278			
Na.	**SUALA AU JAMBO MUHIMU**	**MAONI**	**SABABU**
1.	Kufuta maneno “Executive Director” na District Administrative Secretary katika kifungu cha 7(3) badala yake kuweka maneno “Returning Officer” na kufuta maneno “Ward Executive Officer”katika kifungu cha 7(3) (c) badala yake kuweka maneno Assistant “Returning Officer”.	Tunapendekeza wasimamizi wa uchaguzi na wasaidizi wa wasimamizi wa uchaguzi wawe ni watumishi wa Tume Huru ya uchaguzi walioajiriwa na Tume yenyewe kwa utaratibu wa utumishi wa Tume hiyo.	Wasimamizi wa uchaguzi wakiwa ni watumishi wa Tume ya Uchaguzi itasaidia kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.
2.	Kuboresha utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha Fomu za Tamko la gharama za uchaguzi kwa kumtaka mtia nia kuchukua Fomu za Tamko la gharama za uchaguzi siku anayochukua Fomu za kuomba uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi na kurejesha siku anaporejesha Fomu za uteuzi.	Tunapendekeza kama Sheria ilivyo sasa iendelee, kwa sababu kabla ya kuteuliwa kuwa mgombea anakua hana sababu ya kuwa na gharama za uchaguzi.	Kuteuliwa kwa mgombea kuwe ndiyo Ushahidi wa kumtaka aendeane na Sheria ya Gharama ya Uchaguzi.
3.	Kuweka muda wa Chama cha Siasa kuwasilisha ripoti ya marejesho ya gharama za uchaguzi mdogo.	Tunapendekeza muda unaotumika kuwasilisha ripoti katika uchaguzi mkuu, muda kama huo uwe pia katika	Ili kuwezesha uwajibikaji katika kutoa ripoti ya uchaguzi mdogo, lakini pia itawezesha kufanya

		uchaguzi mdogo.	tathmini ya mambo yote yaliyofanyika katika uchaguzi mdogo.
4.	Kuondoa sharti kwa Vyama vya Siasa kuwasilisha stakabadhi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya uchaguzi.	Tunapendekeza Stakabadhi ziendelee kupelekwa kwa Msajili ili naye ajiridhishe na kuzirejesha katika Chama husika.	Kumwezesha msajili kujiridhisha kama vyama vya siasa vinazingatia taratibu za kutoa na kupokea Stakabadhi.
5	Usimamizi wa gharama za uchaguzi	Uangalizi wa gharama za uchaguzi na ufadhili wa kisiasa inapaswa kuwa chini ya Tume ya Uchaguzi.	Kwa sababu Tume ndio yenye mamlaka ya kusimamia maswala yote ya uchaguzi wanapswa pia kujiridhusha na gharama zote za kuendesha uchaguzi.
6	Usiri kwenye ripoti za ufadhili wa kampeni	i. Vifungu vyote vinavyoweka usiri kuhusu ufadhili wa kampeni viondolewe na uwazi utiliwe mkazo. Uwazi usiishie tu kwenye ufadhili wa kampeni bali uenezwe kwa shughuli zote za ufadhili wa kisiasa na vyama vyote.	Kuhakikisha kunakuwepo na uwazi na uwajibikaji. Wananchi wanayo haki ya kupata ripoti ya uchaguzi.

		ii. Kiwango cha ufichuzi wa ufadhili wa kisiasa kinapaswa kuwa sawa iwezekanavyo na ufichuzi unaohitajika chini ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.	
7	Wagombea waliopita bila kupingwa.	Kuwa na masharti ya wazi na ya udhibiti wa "ugombea bila kupingwa’’ Pia kuwekwa kipengele kinachohitaji kuchunguzwa kwa mgombea huyo ili kupunguza na kuondoa rushwa.	Kuhakikisha udhibiti wa rushwa na takrima kwenye uchaguzi kwa mgongo wa kupita bila kupingwa.

8	Usawa wa kijinsia na ujumuishi.	Sheria inapaswa kuweka masharti ya ndani ya chama kuhakikisha kuwa fedha zimetengwa kusaidia wanawake kugombea nafasi za ndani ya vyama pamoja na ufadhili wa kampeni katika chaguzi za kitaifa. Pia kipengele cha 22 na 23 cha sheria kinapaswa kutoa miongozo ya jinsi vyama vya siasa vinapaswa kutumia fedha/ruzuku kuendeleza ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika vyama vya siasa.	Kuhakikisha wanawake wanashiriki kuwania/kugombea nafasi mbalimbali ndani ya vyama vyao.

3. **SHERIA YA VYAMA VYA SIASA, SURA 258**			
Na.	**SUALA AU JAMBO**	**MAONI**	**SABABU**
1.	Kuzuia mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki shughuli za kisiasa nchini.	1) Neno “kushiriki” litolewe tafsiri kamili bila kuathiri ushirikiano wa vyama vya siasa vya Tanzania na vyama rafiki nje ya Tanzania kwenye programu mbalimbali za kujengeana uwezo. 2) Kushiriki kwa namna yoyote kusizuie mtu kutoka nje ya Tanzania kushiriki kwenye zoezi au tukio kama uchaguzi kwa lengo la uangalizi au kujenga mahusiano na vyama vya Tanzania.	1. Kwajili ya kuondoa utata katika tafsiri unaoweza kuathiri uhuru wa mashirikiano wa vyama vya siasa. 2. Kuendeleza utamaduni wa matizamio katika michakato ya Kidemokrasia.
2.	Kuweka sharti la kuvitaka Vyama vya Siasa	1) Tafsiri za mikutano ya	1) Kwajili ya kuvilazimisha vyama kutoa nafasi kwa

	vyenye usajili kamili kuweka vifungu kwenye Katiba ya kila Chama vianavyotambua Sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalum; kuhamasisha na kuwezesha Vyama vya Siasa kupambana na ukatili wa jinsia na kupiga vita vitendo vya rushwa.	maamuzi ya chama lazima iwe ile ambayo imejumuisha makundi maalumu, na kuzingatia usawa wa kijinsia. 2) Vyama vya siasa vipewe wajibu wa kuhakikisha vinakuza ushiriki mpana wa makundi maalumu katika mipango siku hadi siku. 3) Vyama vya siasa vipewe wajibu wa kutunga sera kali zitakazozuia vitendo vya ukatili wa kijinsia na rushwa ya ngono. 4) Katiba za vyama vya siasa zihakikishe wanaobainika kutenda vitendo vya namna hiyo wanawajibika ikiwa ni pamoja na kutoendelea kushika nafasi	vyama vya siasa kwa makundi maalumu ili yawe sehemu ya maamuzi. 2) Kuweka utaratibu endelevu kwajili kukuza ushiriki wa makundi maalumu. 3) Kujenga mfumo mzuri wa kushughulika na vitendo vya kuzuia ukatili wa kijinsia na rushwa ya ngono. 4) Kutokomeza vikali rushwa ya ngono na vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini, kuongeza uchaguzi kuwa huru na haki kwa wagombea na wananchi kwa ujumla.

		za uongozi.	
3.	Kuweka sharti kukitaka Chama cha Siasa kinachowasilisha maombi ya usajili wa muda kuwasilisha Katiba na Kanuni za Chama husika badala ya sharti hilo kuwekwa katika Kanuni pekee.	Ni pendekezo sahihi. Tunaunga mkono.	Kuweka uimara wa kisheria.
4	Kuweka sharti kwamba, mtu ambaye amepatikana na hatia ya kosa la udhalilishaji wa jinsia asiwe kiongozi wa Chama cha Siasa, ili kudhibiti vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ndai ya vyama vya siasa.	1) Ni pendekezo sahihi isipokuwa hadi pale atakapokuwa amenufaika na haki zake za rufani. 2) Ni muhimu ikawekwa bayana sehemu ambayo kitendo/vitendo hivyo vitakuwa vimetendeka badala ya kubaki kama ilivyo. Mfano; kama ni kwenye chama au ndani ya chama na nje ya chama.	Kudhibiti vitendo vya namna hiyo bila kuathiri haki za wahusika kunufaika na haki zao za rufani. 2) Kwajili ya kuondoa utata.
5	Kuruhusu fedha za ruzuku kugawanywa kwa vyama vya siasa kwa kuzingatia idadi ya kura za Ubunge, idadi ya Wabunge na	Mfumo wa sasa uendelee isipokuwa asilimia 10 ya fedha za ruzuku kwa vyama vya	Kuvifanya vyama kuendelea kutafuta ushawishi ili kunufaika kutokana na mavuna yao ya kiuchaguzi pia kuvijengea uwezo vyama vyenye usajili kamili kujiendesha.

	Madiwani ambao Chama cha Siasa kiao kwa wakati husika na siyo kura za Ubunge, idadi ya Wabunge na Madiwani ambao Chama cha Siasa kilipata wakati wa Uchaguzi Mkuu pekee.	zilizotengwa katika bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha husika igawiwe sawa kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili kamili.	
6	Vyama vya Siasa viruhusiwe kuungana katika miavuli wakati wowote vinapohitaji kufanya hivyo.	Futa ukomo wa muda kwa vyama kushirikiana au kuungana na ruhusu uhuru wa vyama kushirikiana au kuungana wakati wowote wanapoona inafaa kufanya hivyo.	Muda unaowekwa sasa na Sheria ya Vyama vya Siasa kwa vyama kuweza kushirikiana au kuungana unavibana vyama na kufanya kuwe na ugumu kwa vyama kuweza kushirikiana katika uchaguzi.
7	Kuweka masharti yanayofuta vikwazo vya Vyama vya Siasa kupatiwa mafunzo, Elimu au uhamasishaji kutoka kwa mtu au taasisi yoyote nchini.	Kuweka masharti yanayofuta vikwazo vya Vyama vya Siasa kupatiwa mafunzo, Elimu au uhamasishaji kutoka kwa mtu au taasisi yoyote nchini.	Masharti yanayoweka ugumu wa elimu au mafunzo kwa vyama vya siasa hadi ruhusa ya Msajili ya Vyama vya Siasa ni ukiritimba usio na sababu yoyote ya msingi kwa vile viongozi wa Kisiasa ni watu wazima, wenye akili ya kung'amua mafunzo, elimu au uhamasishaji ulio na nia mbaya kwa Nchi yetu.
8.	Utatuzi wa migogoro ya Vyama vya Siasa.	Tunapendekeza kuundwe kwa chombo (Baraza la Usuluhishi wa Migogoro) maalum ndani ya sheria hii litakaloundwa na	1. Kuleta dhana ya usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala kabla ya mahakama. 2. Kuleta dhana ya uhuru wa mchakato wa usuluhishi wa migogoro katika sekta ya vyama vya siasa nchini.

		wajumbe wafuatao; 1. Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania au Mahakama ya Rufani atakayekuwa mwenyekiti wa baraza hilo ambaye atateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 2. Jaji wa Mstaafu wa Mahakama Kuu Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyetiki ambaye atateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. 3. Wajumbe saba (7) ambapo kati yao watatu (3) watakuwa wanawake. **Mamlaka ya Baraza la Usuluhishi wa Migogoro itakuwa ni kusuluhisha;** • Mgogoro kati ya	

		mwanachama na chama cha siasa. • Mgogoro kati ya Chama cha Siasa na Msajili wa Vyama vya Siasa. • Mgogoro kati ya Chama cha Siasa. • Mgogoro kati ya Mgombea Huru na Chama cha Siasa. • Mgogoro kati ya Muunganiko wa Vyama (Coalition) na washirika wake. • Mgogoro kati ya Umoja wa vyama vya Siasa na wanachama wake**.**	

4. SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE, MADIWANI NA VIONGOZI WA SERIKALI ZA MITAA NA VIJIJI YA MWAKA 2023			
Na.	**SUALA AU JAMBO**	**MAONI**	**SABABU**
1.	Kufuta Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kutunga sheria mpya ya Uchaguzi itakayosimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na viongozi wa serikali za Mitaa na Vijiji.	Tunapendekeza kuundwa kwa Sheria moja ya Taifa ya Uchaguzi (The National Elections Act) kusimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na viongozi wa serikali za Mitaa na vijiji.	Uchaguzi wote unapaswa kusimamiwa na kuratibiwa na chombo chenye utaalam, ujuzi, weledi na uzoefu endelevu. Chombo hicho ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi pekee. Ni gharama kubwa kwa Taifa la uchumi mdogo kama Tanzania kufanya uchaguzi miaka miwili mfululizo wakati ipo fursa ya kuunganisha uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za Mitaa.
2.	Kuweka sharti la Uboreshaji wa mara kwa mara wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.	Tunapendekeza masharti yafuatayo ya uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga kura; i. Kusiwe na Daftari la Muda la Wapiga kura, bali kuwe na Daftari la Kudumu kama linavyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	Uchaguzi huru hutegemea uandikishaji maridhawa wa wapiga kura. Kila mtanzania anayo haki ya kuandikishwa na kubaki katika daftari la kudumu la wapiga kura wakati wote akiwa na sifa za kupiga kura.Vijana wanaotimiza miaka 18 wanayo haki ya kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura mara tu wanapotimiza umri wa miaka 18.

		ii. Maboresho ya Daftari la Kudumu la wapiga kura yafanyike mara kwa mara na angalau mara mbili ndani ya miaka mitano. iii. Daftari liwekwe wazi na kufikika kwa njia ya mtandao na nakala ngumu (hard copy). iv. Daftari la Kudumu la Wapiga kura liwe linapatikana, Wananchi wawe na uwezo wa kungalia uhalali wake wa kupiga kura muda wowote.	
3.	Kuweka sharti kwa mgombea wa Ubunge, Udiwani au kiongozi wa Mtaa au Kijiji aliyekosa mshindani katika ngazi yake ya uchaguzi kupigiwa kura ili kupata ridhaa ya wananchi ya kuongozwa naye.	1. Mgombea mwenyewe ndio achukue na kurejesha fomu ya uteuzi na iwapo kuna mazingira hayamuwezeshi kufanya hivyo anaweza kurejesha kupitia mwakilishi. 2. Endapo mtu yeyote ataenda kuchukua na kurejesha fomu bila ridhaa ya mgombea, basi atakuwa ametenda kosa la jinai na kustahili	1. Kuepusha malalamiko ya baadhi ya wagombea kuchukuliwa fomu na kuambiwa fomu zao zimepotea kabla ya kuwafikia. 2. Kuondoa uwezekano wa watu wenye hila kuweza kuwachukulia wagombea fomu na kuwajazia vibaya ili waenguliwe na Tume. 3. Kuondoa hila ya kuwaonea baadhi ya wagombea kwa kuwakatalia kupokea fomu kutokana na makosa madogo madogo ya kiuchapaji. 4. Kuondoa hisia ya baadhi ya wagombea kuenguliwa kwa uonevu. 5. Kukomesha vitendo vya mgombea fulani kutoa rushwa kwa

		kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. 3. Fomu zote za uteuzi kwa ngazi ya Urais, ubunge na Udiwani zijazwe kwa ukamilifu na ufasaha na kurejeshwa. Endapo kutatokea hitilafu kwenye fomu na nyaraka ambatishi Mgombea Husika awe na fursa ya kurekebisha hitilafu hizo na kurejesha tena fomu zake. 4. Mgombea yeyote hatokosa sifa ya kuteuliwa kwa sababu ya hitilafu ya ujazaji wa Fomu bali Tume itoe nafasi ya urekebishaji wa Fomu na uteuzi kufanyika. 5. Mgombea atakayeshindwa kurejesha fomu kwa makusudi atachukuliwa kuwa anafanya mzaha na mchakato wa uchaguzi na atachunguzwa na Tume ikishirikiana na Takukuru ili	wagombea wenzake ili wajiondoe katika kinyang'anyiro cha kugombea nafasi husika. 6. Kuweza kubaini wagombea wanaofanya mzaha na michakato ya Uchaguzi na kuwachukulia hatua ili kukomesha mizaha yao. 7. Kukomesha tabia ya wasimamizi kufanya hila ya kuondoka ofisini ili baadhi ya wagombea wasiwakute wakati wa kurejesha fomu zao. 8. Kuondoa malalamiko ya baadhi wagombea kutompata msimamizi wa Uchaguzi wa kuweza kumkabidhi fomu wakati wa kuzirejesha baada ya kukamilisha ujazaji wa maombi ya uteuzi.

		kubaini vitendo vya rushwa. 6. Mgombea atakayebainika kushindwa kurejesha fomu kwa makusudi ili kumfanya mgombea mwenzake awe amepita bila kupingwa ataadhibiwa vikali kwa kuzuiwa kugombea nafasi yoyote katika kipindi cha miaka 20. 7. Mgombea anayefika ofisi ya msimamizi wa Uchaguzi kurejesha fomu na kutomkuta atachukuliwa kuwa amewahi muda wa kurejesha fomu hata kama msimamizi atarejea ofisini nje ya muda. 8. Ili kufanikisha malengo ya Sheria hii na kulinda haki ya mtu kuchagua kiongozi anayemtaka hakutokuwa na mgombea atakayepita bila kupingwa.	
4.	Kuweka utaratibu wa kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Mbunge, Diwani au kiongozi wa Mtaa/kijiji mteule.	**Tunashauri Masharti yafuatayo:** 1. Mgombea wa kiti cha mbunge anayewakilisha jimbo la uchaguzi,	1. Demokrasia ya kweli inataka uchaguzi wenye mashindano siyo kupita bila kupigiwa kura.

		mgombea wa kiti cha diwani anayewakilisha Kata na mgombea wa ngazi ya uongozi katika serikali za mitaa au kijiji apigiwe kura ili kupata ridhaa ya wananchi wa Jimbo, Kata, Mtaa au kijiji atakayoiwakilisha. Sharti hilo pia lipo kwa upande wa Mgombea wa Urais chini ya Fungu la 44 la Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Kusiwe na mbunge au diwani anayewakilisha jimbo, Kata au Mtaa/Kijiji ambaye atatangazwa ameshinda bila kupigiwa kura. Hata hivyo, Mahakama Kuu kwenye shauri la Kikatiba (**Joran Lwehabura Bashange vs The Chairman of National Electoral Commission and Another, Miscellaneous Civil Cause No. 19 of 2021**) imeshatamka wagombea waliopita bila kupingwa bila	2. Dhana ya kupita bila kupingwa ni batili na inafifisha maana nzima ya uchaguzi.

		kupigiwa kura ni kinyume cha Katiba na imefuta/kubatilisha. Pendekezo mbadala: Inapotokea mbunge, Diwani au kiongozi wa mtaa/kijiji mteule amepoteza sifa, Tume ya Taifa ya uchaguzi imtangaze mtu aliyepata kura zilizomfuatia mshindi kuwa ndiye kiongozi mteule na kuwa atatumikia kwa kipindi chote kilichosalia kabla ya uchaguzi unaofuata.	Sababu zake a. kuleta uwiano wa mfumo wa uchaguzi kwa nafasi zote kama ilivyo kwa urais b. Kuepuka gharama za mara kwa mara za kurudia uchaguzi pale viongozi wateule wanapopoteza sifa ikiwemo kufariki dunia.
5.	Mgombea Huru au Binafsi aruhusiwe katika Uchaguzi kwa ngazi ya Rais, Ubunge, Udiwani na Serikali za Mitaa/Vijiji.	Iruhusiwe kuwa Mtu yeyote anayetaka kuomba ridhaa ya Watanzania kuweza kuwaongoza aruhusiwe kufanya hivyo ama kwa kudhaminiwa na Chama cha Siasa, Muungano wa Vyama au	6a. Kuzuia mgombea huru au binafsi ni kuminya haki ya Kikatiba na Kisheria kwa Mtanzania kuweza kuomba kuchaguliwa kuwa kiongozi bila kupitia Chama cha Siasa. Uminyaji huu wa Haki umekemewa na kubatilishwa na hukumu ya kesi ya Mgombea Binafsi katika ngazi ya Mahakama Kuu na baadaye Mahakama ya

		wadhamini huru wasiowakilisha chama cha siasa ili mradi ni wapiga kura walioandikishwa katika daftari la kudumu la mpiga kura.	Afrika na kuruhusu Mgombea huru ni utekelezaji wa hukumu hizo za Kimahakama.
7.	Sheria iweke Masharti yanayoweka mfumo utakaopaswa kufuatwa na vyama vyote vyenye usajili kamili katika kupata wagombea wa Ubunge na udiwani wanawake wa Viti Maalum.	Sheria iweke Masharti yanayoweka mfumo utakaopaswa kufuatwa na vyama vyote vyenye usajili kamili katika kupata wagombea wa Ubunge na udiwani wanawake wa Viti Maalum.	Hii italeta uwiano wa vyama katika utaratibu wa kupata Wabunge na Madiwani wanawake wa Viti Maalum badala ya utaratibu wa sasa ambapo vyama vinatumia mifumo na utaratibu usiofanana kinyume na maelekezo ya ibara ya 81 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
5. SHERIA YA ELIMU YA URAIA YA MWAKA 2023			
1.	Itungwe Sheria Mpya ya Elimu ya Uraia itakayoweka mfumo, utaratibu, mamlaka na miongozo ya namna ya utoaji wa Elimu ya Uraia na jinsi inavyotofautiana na Elimu ya Mpiga Kura Nchini	Itungwe Sheria Mpya ya Elimu ya Uraia itakayoweka mfumo, utaratibu, mamlaka na miongozo ya namna ya utoaji wa Elimu ya Uraia na jinsi inavyotofautiana na Elimu ya Mpiga Kura Nchini ambayo ni jukumu la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.	Kutungwa kwa Sheria ya Elimu ya Uraia kutaondoa ombwe la kutokuwepo kwa Sheria inayoongoza Elimu hiyo Nchini na hivyo kumaliza mkanganyiko uliopo kati ya Elimu ya Uraia na Elimu ya Mpiga Kura Nchini.

	ambayo ni jukumu la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.		
2.	Sheria ya Elimu ya Uraia iwataje wadau wote Muhimu ikiwa ni pamoja na Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini na taasisi nyinginezo zenye uwezo wa kutoa elimu huru ya Uraia bila kuegemea upande wowote kisiasa.	Sheria ya Elimu ya Uraia iwataje wadau wote Muhimu ikiwa ni pamoja na Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini na taasisi nyinginezo zenye uwezo wa kutoa elimu huru ya Uraia bila kuegemea upande wowote kisiasa.	Hii itaondoa utata uliopo sasa juu ya nani anapaswa kutoa Elimu ya Uraia Nchini.

C. HITIMISHO

Kwa ujumla, NaCONGO tunaona kuwa hii ni fursa muhimu na nzuri ya kuboresha mifumo ya usimamizi wa Uchaguzi na uratibu wa Elimu ya Uraia na Elimu ya Mpiga Kura Nchini ambayo imejitokeza na ambayo haipaswi kuchezewa. Aidha, Mashirika wanachama wa NaCONGO tunaamini kuwa maoni yetu yatachangia katika kazi ya kuboresha sheria mbalimbali zenye mapungufu na katika utungaji wa Sheria Mpya katika maeneo ambayo yanahitaji wa mfumo mpya wa Kisheria. Kwa sababu hizi na nyingine ambazo hatukuzitaja hapa, tunapenda kushukuru serikali kupitia Msajili na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kutupatia mwaliko huu mahsusi kuwasilisha maoni haya. Tunapenda kuwashukuru wadau wote waliojitoa kuweza kuwasilisha maoni kwetu katika muda mfupi ambao tulikuwa nao. Tunaamini kuwa tutaendelea kushirikishwa katika hatua za baadaye za utungaji na uboreshaji wa Sheria tajwa hapo juu. Mwisho, tunapenda kuweka bayana kuwa mambo kadhaa tuliyoyapendekeza yanataka zaidi ya mabadiliko ya Sheria. Tunashauri kuwepo Mchakato wa Marekebisho ya 15 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwianisha masuala ya kisheria yaliyopendekezwa kuboreshwa na ibara husika za Katiba ya Nchi.

D. VIAMBATANISHO

Tafadhali rejea viambatanisho vifuatavyo kwa ufafanuzi na taaria zaidi kuhusu mapendekezo ya wadau kama ifuatavyo;

1. Sheria ya Mfano ya Uchaguzi.
2. Sheria ya Mfano ya Vyama vya Sisasa.